

## **USAHIHI WA KAULI YA MH. RAIS JUU YA MISHAHARA YA WATUMISHI**

Kumekuwa na upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu kuhusiana na hotuba na Rais Dkt Magufuli aliyoitoa katika ufunguzi wa Mkutano wa 33 wa ALAAT hasa kuhusu suala la upandishaji wa mishahara kwa watumishi wa umma.

Kwanza ieleweke katika Mkutano ule madiwani walimuomba Rais Dkt Magufuli awaongeze posho zao. Majibu ya Rais Dkt Magufuli katika hilo lilikuwa ni hawezi kuwaongezea posho madiwani hao kutokana na moja ya masharti ya kugombea udiwani lazma awe na shughuli inayomuingizia kipato kwakuwa udiwani sio kazi inayoingiza kipato bali ya kuwahudumia wananchi. Rais Magufuli akaendelea na kuwaambia madiwani kuwa kwasasa hawezi kuwaongezea madiwani posho zao kutokana na changamoto za kimaendeleo zilizopo kwenye halmashauri na kuwaomba ushirikiano badala ya posho hizo walizoomba kuongezewa basi wazielekeze kwenye mambo ya maendeleo (madiwani walipiga makofi mazito)

Cha kushangaza watu wamebeba hilo neno na kuanza kupotosha kuwa serikali imesema haitapandisha mishahara kamwe. Hili jambo sio kweli.

Wacha leo nitoe somo kuhusu kupanda kwa mishahara ya watumishi na watanzania muelewe na muachane na ushenzi wa wapinzani uchuro.

### **NAMNA MISHAHARA INAVYOPANDA**

1. Kupanda daraja - kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma Na. 8/2002 imeweka wazi kuwa mtumishi atapanda daraja la kazi kutokana na kujiongeza sifa, ujuzi na uzoefu. Sharia imeendelea kuweka wazi kuwa mtumishi aliyepanda daraja atalipwa mshahara wa ngazi ya daraja lake jipya.
2. Utaratibu wa kawaida wa serikali kupandisha mishahara kila mwaka(annual increment) – Sheria ya Utumishi wa umma Na.8/2002 imeweka wazi pia kuhusu ongezeko la mishahara kwa wafanya kila mwaka kutokana hali ya kiuchumi wa nchi hasa mfumuko wa bei nchini (Kuongezwa kwa mshahara kutokana na mfumuko wa bei kunamuwezesha mtumishi kuhimili ukali wa maisha unaosababishwa na mfumuko wa huo)
3. Kupungua kwa kodi ya mshahara(PAYE) hii hufanya mtumishi kupokea kiasi kikubwa cha pesa tofauti na awali ambapo kodi ya mshahara inakuwa kubwa.
4. Kuongeza kwa kima cha chini cha mshahara madaja ya mishahara mingine.

### **HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI JUU YA KUPANDISHWA KWA MISHAHARA.**

Ni ukweli usiopingika kutokana na kusheheni kwa watumishi hewa pamoja na watumishi wa serikali wenye vyeti feki iliizimu serikali kusitisha upandishwaji wa madaraja kwa watumishi pamoja na ongezeko la mwaka la mshahara kwa watumishi kwa kipindi cha mwaka mmoja tu. Lengo lilikuwa ni

- i. Kuboresha Utumishi Kazini.
- ii. Kuokoa Fedha za Serikali zinazotumika Kulipa Wasiostahili kuelekezwa katika mambo ya maendeleo
- iii. Kuwa Na Watumishi Wanaofanya Kazi Kwa Mujibu Wa Weredi Na Fani Zao.

### **UPANDISHAJI WA MISHAHARA**

1. Mwaka 2016 serikali ilipunguza kodi ya mshahara(PAYE) toka asilimia 11 mpaka asilimia 9 hivyo kupungeza kipato cha mtumishi tofauti na awali
2. Baada ya zoezi la kuondoa watumishi hewa pamoja na watumishi wenye vyeti feki serikalini, Kuanzia mwezi wa Julai, 2017 serikali kupitia kwa Waziri wa Tamisemi anayeshughulikia Utumishi ilitangaza kupandisha madaraja watumishi zaidi ya 193,000 kwa mwaka 2017/2018 na tayari watumishi wameanza kupandishwa madara kuanzia mwezi julai na wanalamba mishahara mipya ya juu kabsa.
3. Mwezi julai 2017 Serikali ilitangaza kuanza kutoa nyongeza ya mishahara ya kila mwaka ambayo imeshaanza kutolewa. Agosti, 2017 annual increment ilishaanza kulabwa na watumishi wa umma.
4. Mwezi Julai, 2017 serikali iliweka wazi azma yake ya kupandisha mishahara(ngazi mbalimbali za mishahara) kuanzia bajeti ijayo yaani mwakani.

Hii ndio Tanzania mpya yenye ukweli na uwazi. Watumishi wa Umma endeeleni kufanyakazi ya kuleta maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

\*Uzalendo kwanza, Naipenda Tanzania \*